



# DONE (IMEKWISHA)

*Na Francois du Toit*

□ Hakimiliki 2010

(Unahimizwa kusambaza kwa uhuru - tazama ukurasa wa mwisho kwa maelezo)



## IMEKWISHA (Swahili)

### ULINGANIFU MZURI WA WAKATI WETU

“Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana” Ebr.11:1. Kutumia vema maneno ya wakati ni suala muhimu shuleni kwa kila mwanafunzi wa lugha; hata hivyo hatuwezi kufanikiwa tukiutumia vibaya katika kutafuta kuupata ufunuo wa imani. Wayahudi walikuwa wameshikwa sana na maneno ya wakati ujao, hata kumkosa Masihi kati yao! Hata baada ya miaka elfu mbili, bado wanamngojea! Wakristo wengi leo wameshikwa na mtego ule ule. Pia kupitia baadhi ya nabii binafsi zinazoendelea kuwafanya wafurahie wakati ujao, au kufasiri kuja kwa Yesu mara ya pili kama ndiyo wokovu wao kutoka katika uovu wao, kana kwamba kuja kwake mara ya kwanza kulishindwa!

Katika maelezo yetu kuhusiana na wakati, tunashindana na maandiko kama hili la Rum.4:17, “Mungu mwenye kuwahusisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako!” Pia katika kujifunza unabii, tunashangaa, kwa nini manabii wanaongea katika usemi wa wakati uliopita wakitabiri juu ya mateso ya Kristo miaka 700 ikiwa mbele. “Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona” Is. 53:5. Ndipo Yesu anaibua wazo la maombi katika Marko 11:22,24. “Mwaminini Mungu” Anasema, “Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.” (Hakuna kuomba-omba, hakuna kusihii!) Alipokuwa amesoma moja ya nabii maarufu, anahitimisha mazungumzo yake kwa maelezo, “Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu!” Luka 4:16-21. Wakati mwanamke msamaria anaanza kulinganisha juu ya desturi za dini, alimshangaza mwanamke kwa kufunua kwamba saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu wa Samaria, wala Yerusalemu; waabudu halisi, watamwabudu katika roho na katika kweli. (Kuabudu kote kwaweza kuwa kwa dhati, lakini si kuabudu kote ni kweli!) Yohana 4:21,23. Ni dhahiri kwamba, ikiwa Yesu ndiye utimilifu wa wakati kweli, kila tafsiri inayowezekana katika maisha yetu inatiwa changamoto sawasawa na maneno “sasa ile imani imekuja.” Gal. 3:23-26 na 4:1-4.

### SHERHE YA UKAMILIFU

Siku moja nilipata hamasa ya kumchukua mpiga picha maarufu katika safari ya mashua ya maonyesho, kule Walker Bay. Niliweza kujua kutokana na aina ya kifaa cha Kamera yake kwamba hakuwa mtalii wa kawaida. Alinieleza kuwa alihitaji kuchukua picha mbili tu kwa mwaka ili kukidhi mahitaji yake! Nilivutiwa sana kumwangukia msanii yule akiwa kazini. Kwa wepesi na ujuzi aliweza kubadilisha lensi na mikanda bila kupoteza wakati. Tukiwa njiani kurudi bandarini tuliona kundi la mamia ya ndege walao samaki (mnandi). Mara wote waliruka; mlio na sauti za mabawa yao zilikuwa kama ngoma zikiitikia juu ya maji. Mpiga picha wetu aliwanasa kwa picha kwa furaha na mara alipaza sauti: “Nimepata, Nimepata!” Ilikuwa ni ajabu kushuhudia furaha katika uso wa mtu yule. Alijua kwamba alikuwa amenasa muda ambao huenda ulikuwa wa thamani kuliko vifaa vyake vyote alivyovikusanya. Nilimwangukia akiwa amestarehe na kupumzika na kuelewa kuwa Sabato ilikuwa ni sherehe ya ukamilifu, wala sio mapumziko kutokana na ratiba nzito ya kushika desturi za dini! Mw. 1:31. Wakati alipokuwa akiweka vifaa vyake kwa uangalifu, nilishikwa na wazo la picha; mwanga wa ghafula ajabu, umbo, mwendo na rangi zikinaswa na kuhifadhiwa katika mkanda ili kutolewa bila kujali wakati, na kung'aa juu ya kurasa za

magazeti. Sehemu za maonyesho ya picha hizi zingefurahiwa na kila mila au lugha, na wakati wowote ujao. Nilifikiria jinsi ambavyo msanii huyu angehifadhi thamani hizi kwa namna ambayo hakitapotea kitu katika picha ya asili; bila kujali nini kingetokea kwa wapiga chapa, kama zingetengenezwa, kusahauliwa au kuharibiwa. Kama vile maneno yanavyoweza kuhifadhi maumbo yaliyo na uzuri adimu, ili yaweze kurudiwa kwa wakati wowote, katika lugha au wazo lolote.

Katika moja ya hadithi zake bora, msanii Gentian Hill, Elizabeth Goudge, anaitia rangi ya mtoto mdogo Stella akimsikiliza baba yake wa kambo alipokuwa anasoma Biblia: "Ndani ya kitabu chote, hata katika sehemu za kutisha, sasa na kuendelea, ghafula lugha itamuathiri kama vile uchawi. Hali ya kipekee ya kutolewa kwa Baba Sprigg haikumtisha hata kidogo. Ilikuwa kama vile sauti yake kali ikirusha maneno ovyo hewani ikitenganisha sehemu ndogo-ndogo zisizo na maana, na mara huanguka tena na kubadilika, kama mlio wa kengele au matone ya mvua yakilengwa pamoja na mwanga wa jua na kuona sura ya nchi yenye uzuri usio na kifani ukifunguliwa akilini. Lili kuwa jambo la siri kwa Stella kuona kwamba ni maneno tu yalifanya haya kutokea. Alidhani kuwa mtengenezaji wa maneno haya aliyafanya ili kushika maono yao kama mmoja afanyavyo sanduku ili kutunzia hazina, na sauti ya Baba Sprigg ilikuwa ni ufunguo ukisugua ndani ya kufuli, ili kwamba sanduku lifunguke na kuwaweka huru. Yale madiliko katika hewa bado yalibaki kama kitu kisichoelezeka, kama mabadiliko ya ghafula ndani yake, wakati wa kutokea ajabu, akili yake iliyolala iligeuka mara na kumetameta kwa ajabu, na roho yake iliruka-ruka ndani yake kama ndege..."

Kwa mara ya kwanza katika umri wa dunia, Muumbaji asiyeonekana aliweza kuonyesha sura yake na mfano wake katika umbo la kuonekana, Mwanzo 1:26. Uumbaji wa utukufu na ukamilifu uliweza kuhifadhiwa kwa ajili ya milele katika Neno ambalo lilikuwako tangu mwanzo, ijapokuwa Adamu alikuwa ameanguka. Sulemani aliliona jambo hili katika Mith. 8:22-25,30; "Bwana alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, Kabla ya matendo yake ya kale. Nalitukuka tokea milele, tangu awali, kabla haijakuwako dunia. Wakati visipokuwako vilindi nalizaliwa, Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji. Kabla milima haijawekwa imara, kabla ya vilima nalizaliwa. Alipokuwa hajaumba dunia...Nikawa furaha yake kila siku; Nikifurahi daima mbele zake." Thamani yako ya asili, kwa jinsi ambavyo Mungu alikuwako kabla hajakuumba katika tumbo la mama yako, bado ni kamili! Kwa njia ya mahubiri ya Injili ya kweli, mwujiza wa ule wakati wa milele umefunuliwa tena katika uso wa Kristo kama vile katika kioo, ili kwamba nuru ya uzima iweze kupambazuka ndani yetu, na tuweze kumtazama uso kwa uso, na kwamba tuweze kujijua sisi wenyewe kama vile tunavyojuliwa. 2Kor. 4:2-7; 1Kor. 13:10-12.

## SISI TU WAZAO WAKE KWELI

"Mpeni ukuu Mungu wetu, Yeye Mwamba, kazi yake ni kamilifu!" Kumb. 32:3,4. "Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu." Ef. 2:10. "Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyooonekana...vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye." Kol. 1:15-17. Injili haiwezi kuufunua ukombozi au upatanisho ulio na maana ya chini kuliko huu: "Akiisha kutujulisha siri ya mapenzi yake, sawasawa na Uradhi wake, alioukusudia katika yeye huyo; Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia." Ef. 1:9,10. "Kila kitu kilichoko mbinguni au duniani kinapata ukamilifu na utimilifu wake katika yeye." (tafsiri ya Phillips). "Yaani Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na

nafsi yake, asiwahesabie makosa yao.” 2Kor. 5:19. Ukamilifu huo ulitangazwa na kusherehekewa katika Sabato ya Mwanzo 1 na 2, sasa umefunuliwa katika ukombozi na kufanyika kuwa muhimu kwa mahitaji yetu ya kibinadamu, ili kuingia katika pumziko la Mungu, kuona kama Mungu aonavyo ili kujua pamoja naye, na kwa hiyo kuachana na kazi zetu sisi wenyewe! Sef. 3:17. Hatuwezi kufanikiwa tunapooona upungufu katika wokovu kuliko Mungu anavyoona ndani yake! “Sisi je, tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii?” Waeb. 2:3. Tunawezaje kuutukuza ukombozi ikiwa nusu hawajaambiwa juu ya hekima ya Sulemani? Na mkuu kuliko Sulemani amekuja! Luka 11:31.

Katika hotuba yake maarufu kule Athens, (Mdo 17) Paulo anawakumbusha mataifa wenye elimu ya juu kwamba, Mungu wanayemwabudu bila kumjua, ni Mungu aliyumba ulimwengu na vyote vilivyomo, “Kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono; wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu chochote; kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote. Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao; ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone; ‘Yeye ndiye sifa yao ya kweli’ (Kigriki, *psallo*, kugusa waya kwa ajili ya kufanya muziki), ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu, (hayuko karibu kwa Wayahudi kuliko alivyo kwa Mataifa!) kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu... maana sisi sote tu wazao wake.” Alikibomoa kile kiambaza kilichotutenga, Ef. 2:13-16. Asili yetu ndani yake inafunua utambulisho wetu wa kawaida, Ebr. 2:11. Mungu sio mzao wa makisio bora ya mwanadamu; Yeye ni mkuu kuliko kosa kubwa la kidini au mtu mwenye uwezo wa kushawishi katika kujaribu kumwelezea Mungu. Yu mbali na kufa au vitisho, na kamwe hawezi kupunguzwa kwa ujuzi wetu au maelezo ya ujinga wa elimu ya juu au elimu stadi. Imani yetu siyo tunda la uvumbuzi au fikira zetu wenyewe, bali ni kuakisi kama kwa kioo kwa ubunifu wake uliofunuliwa katika nafsi ya Kristo. Mungu alikatiza historia ya mwanadamu, wakati kwa mara ya kwanza tangu Adamu, mng’ao wa sura na mfano wake, ulipotokea tena bila waa wala kosa katika umbo la mwili, onyesho la tabia na kuwepo kwake. Ebr. 1:3; Kol. 1:15,16. “Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya mwili...Na ninyi mmetimilika katika yeye.” Kol. 2:9,10. (tafsiri ya Phillips). “Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu!” Mdo 17:22-31. Hukumu ya wanadamu ilianguka juu ya mtu mmoja; ufufuo wake kutoka kwa wafu ni ushuhuda wa milele wa kuachiliwa kwao. Ndiye peke yake astahiliye kuwakilisha ubinadamu na Uungu katika nafsi yake mbele ya mahakama kuu ya haki. “Tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote 1Yoh. 2:1,2. “Alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki. Rum. 4:25.

## UZIMA UMEPAMBAZUKA

Miaka sitini baada ya kumwona Yesu katika mwili kwa mara ya mwisho, Yohana, umri wake ukiwa katika miaka ya tisini, anaeleza juu ya siri ambayo ilifunuliwa na kubadilisha maisha yake kutoka hali ya kuwa mvuvi asiye na elimu, na kuwa mtu mtakatifu. Sehemu kubwa ya maisha yake ya baadaye (kama miaka 30) aliishi katika Asia ndogo, na hasa katika Efeso; kwa hiyo, msisitizo mkubwa wa mafundisho ya Paulo unalenga kutokana na maandishi ya Yohana. Haya aliyafanya ama kutokea

Efeso au kutokea kisiwa cha Patmo mahali alipoishi miaka michache ya uhamisho. (Linganisha Kol. 1:15-17; Yoh. 1:1-3,16,17; 1Yoh. 5:20). Anaelewa kwamba Neno lina asili ya milele na hatima yake ambayo kamwe haiwezi kufungiwa katika kisiwa chenye upweke, au ujuzi; wala Neno haliwezi kutegwa kwa mafundisho ya wanadamu au desturi. Hakuna tafsiri dhaifu au ukalimani ambao ungeweza kupunguza kusudi la Mungu la asili.

Uadilifu thabiti wa wazo la Mungu utahifadhiwa milele na kusherehekewa kutika kufanyika mwili kwa Yesu; maisha ya wanadamu kuwa na hatima ya Neno isiyodakizwa.

Zingatia jinsi Yohana anavyotumia mara nyingi neno, *ginomai*, maana yake kuzaliwa au asili: "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Vitu vyote vilifanyika (Gr. *Ginomai*, kutoka *genos*, kutoa uzao) kwa huyo. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza. (Gr. *kata+lambano*, kuchukua kwa nguvu, kunyakua) Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu amekuja ulimwenguni. Ulimwengu uliumbwa (Gr. *ginomai*) na yeye, wala ulimwengu haukumtambua. Alikuwa kwake, wala walio wake hawakumpokea (Gr. *para+lambano*, kutwaa, kushirikisha na). Lakini kila mmoja anayemtambua kuwa ndiye asili yake ya kweli, (Gr. *lambano*, kutambua, kutwaa, tambulikana kwa), ndani yao anathibitisha uadilifu wa uwana wao, (Gr. *didomi*, katika suala hili, kutoa kitu kwa mtu ambacho tayari ni mali yake, hivyo ni kurudisha) ukweli kwamba tayari ni mali yake, wamezaliwa kutoka juu. Wana mwanzo wao na kuwapo kwao ndani yake! (Gr. *eksousia*, uadilifu, uhalali, mamlaka, misingi halali). Yesu amekuja kudhihirisha uwana wa kweli wa mtu; Alithibitisha asili yetu na mpango wake, 'Naye Neno alifanyika (Gr. *ginomai*) mwili, na sasa anakaa ndani yetu!' Yohana 1:1-14. "Hatuhubiri amri mpya, ila amri ya zamani mliyokuwa nayo tangu mwanzo. Tena nawaandikia amri mpya, neno lililo kweli ndani yake na ndani yenu, 1Yohana 2:7,8. Ndani yake tunatambua kuwa hatupo hapa kwa fursa au bahati mbaya; au kwa matakwaa ya mzazi wa kidunia, wala hatujawa uzao wa kimwili tu; tumekuwapo kwa udhihirisho wa shauku ya Mungu kujifunua katika mwili. Umilele wake, Neno lisiloonekana, wazo lake la Roho, lilifanyika (Gr. *ginomai*, kuzaliwa) mwili. Yakobo anasema, 'Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa Neno la kweli...Mtu yeyote asikiaye Neno hili, anaona sura ya kuzaliwa kwake kama vile katika kioo, anajiona kama alivyo kutoka katika mtazamo wa Mungu.' Yak. 1:17,18,23.

Kamwe Mungu hakulichanganya wazo lake la asili. Neno lilifanyika mwili na kufanya makao (akakaa) ndani yetu, tulitazama na kuona ajabu juu ya siri ya hitimisho letu ndani yake; (*theomai* kutazama kwa mshangao, kutambua) Nasi tukauona utukufu wake (Gr. *doxa*, onyesho la wazo lake), utukufu kama wa asili, aliyezaliwa na Baba kwa uthabiti, aliyejaa neema na kweli.' (Nia ya asili, au wazo la Mungu, uliotunzwa, na sasa umefunuliwa katika Kristo. Yuko katika nafasi zote 'mwana pekee,' *monogenes*, ni kama muundo thabiti wa asili, kama vile alivyo mzaliwa wa kwanza katika wafu. Kol. 1:18; 1Pet. 1:3). Tumekwishatambua kwamba yeye ni ufunuo wa ukamilifu wetu. Kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema.' Gr. *garin anti garitos*, neema tusiyoistahili) 'Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo. Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee (asili, thabiti) aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.' Yoh. 1:1-5, 9-14, 16-18. "Neno lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia kwa habari ya Neno la uzima; hilo tuliloliona na kusikia, twalihubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana na nasi. Hilo tulilolitazama na mikono yetu ikalipapasa, ndiyo uzima uliopambazuka! (Gr. *psallo*, kugusa uzi wa chombo cha muziki, hivyo kutoa mlio). Uzima ule uliokuwa na Baba tangu mwanzo, sasa umepambazuka juu yetu! Uzima wa Baba usio na mwisho ulionekana mbele ya

macho yetu katika hali ya mwanadamu! Sasa, uzima huu unafafanuliwa katika muungano wa ushirika na Baba na Mwana usio na mipaka wala kukatizwa. Katika miaka yote tangu kupaa kwa Yesu, Yohana anaendelea kuufurahia urafiki na Mungu, na anataka kuuendeleza ushirika huu usiozuilika kwa njia ya maandishi yake kwa kila mwamini; "Ili furaha yetu itimizwe." 1Yohana 1:1,2,4.

*Je, mvua ina baba?*

*Ni nani aliyeyazaa matone ya umande?*

*Ni nani aliyeyazaa asubuhi?*

*Alifanya mapambazuko kuijua sehemu yake?*

*Umeyafahamu mapana ya dunia?*

*Je, unaujua mwanzo wake?*

*Anakujua kwa jina*

*Mpango wake ndiyo madai yake*

*Anatangaza kwa ushujaa, "Nipime"*

*Je, umeupima moyo wako?*

*Je, umepima ukuu wa kuwapo kwako?*

*Amekuchagua kukaa katika utimilifu wa ndoto yake*

*Je, umeelewa? Yuko nyumbani ndani ya moyo wako*

*Jengo la kuishi ndani yako lisilo na kuta*

*Uchukue upendo wangu mpaka mwisho*

*Upeleke upendo wangu kwa kila mtu*

*Zihesabu nyota, uhesabu mchanga, yapime mataifa katika mkono wangu*

*Njoo sasa, unipime*

*Ninautimiza umilele wako (Anthea van der Pluym ACTS TEAM)*

## MWANA WA ADAMU NI MWANA WA MUNGU

Neno la Mungu la milele limefungwa katika ufunuo wa uwana wetu. Hivi sasa, Yesu ni kielelezo kamili katika nafsi moja kwa maeneo yote ya wazo la Mungu kuhusu utambulisho wa mwanadamu wa kweli na ukombozi, kama ulivyoelezwa katika torati na manabii. "Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu wake huko juu; Ubinadamu wake unawakilisha kutokuwa na hatia sisi! Mara moja kwa wote, alituweka huru kutokana na hatia ya dhamiri! Ebr. 1:1-3; 9:6-14; 10:1-3,10,14. "Ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika." Kol. 2:3,9,10. (Kufanyika mwili kwake kunafungua siri ambayo inafunua siri ya kuunganika kwa mwanadamu katika Kristo. Kifo chake kinatangaza ukweli kwamba, "Tulikufa, na uhai wetu ulifichwa pamoja na Kristo katika Mungu." Kol. 3:3). Yeye ni kiini cha maandiko! Mungu alitushirikisha katika Kristo kabla ya msingi wa dunia! Ef. 1:4. 'Ni kutoka kwake tunapata asili yetu' 1Kor. 1:30. Knox.

Ni jambo la utukufu kutambua kwamba mtiririko wa kweli wa maandiko sio wa kihistoria au mambo ya desturi, bali ni uhusiano mkubwa ulio halisi, yaani uwana wetu! Ebr. 1:1,2. Maandiko yote yanaonyesha ushirika unaohusiana na ufunuo wa Kristo tu, ambao hakika unamwakilisha mwanadamu; ndiye utambulisho wetu wa kweli!. "Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia." Yoh. 5:39. Maandiko yanatuonyesha kwa Kristo, na Kristo anatumia! "Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa

utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo." 2Kor. 3:18. Tunaposoma maandiko sawasawa na ukombozi, Biblia inafanyika kuwa kitabu kipya. "Kwa maana andiko huu, bali roho huhuisha;... maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima." Yoh. 6:63. Biblia imewachanganya na kuwagawa watu wengi zaidi kuliko kitabu kingine chochote, na bado ujumbe wake wa kiroho umebakia na ukamilifu wa milele katika huyo mmoja; Neno lililofanyika mwili, anamfunulia kila mtu! "Ninyi mkikaa katika Neno langu (Neno lililokuwako tangu mwanzo, Neno ambalo ni Mungu, Neno lililofanyika mwili na kukaa ndani yetu), tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru. Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli." Yohana 8:31,32,36. Uhuru wa mwanadamu uko katika kutambua uwana wao wa kweli! Huu ndio ukweli kama ulivyo katika Kristo. Ef. 4:21. Kama alivyo, ndivyo tulivyo katika ulimwengu huu." 1Yoh. 4:17. Kujua ukweli kuhusu sisi tulivyo kama ulivyofunuliwa katika Kristo, ndio unaotuweka huru kuwa vile tulivyo. Yeye siyo mfano kwa ajili yetu, bali ni mfano wetu! Imani pekee iliyo ya thamani ya kuifuatia ni imani ya Mungu; anachokiamini Mungu kutuhusu sisi, ni kustahili kwa utumishi wetu usiogawanyika. Imani ya Mungu inaonyeshwa katika ubinadamu, uzima, kifo na ufufuo wa Kristo. Mungu anathamini kuunganika kwetu ndani yake! 'Imani huja kwa kusikia kunakotokana na ufunuo wa Kristo.' Rum. 10:17. (Tazama tafsiri iliyosahihishwa). Kulitukuza andiko lolote nje ya mtiririko wake wa kweli, ufunuo wa Kristo ndani yako, ni kuzunguka katika fadhaa na makosa.

"Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu (sheria na kanuni maarufu zilizokubalika) wala si kwa jinsi ya Kristo. Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya mwili. Na ninyi mmetimilika katika yeye." Kol. 2:8-10. Pia tazama mistari ya 16-23, mifano yote na vivuli vya agano la kale, sasa vimebatilishwa na uhalisi mkuu, uumbaji mpya katika Kristo! "Kwa kuwa torati ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo." Ebr. 10:1. "Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu. Aliumba katika yeye mtu mpya mmoja! Ef. 2:10,15; 2Kor. 5:14,16,17.

## YESU — KUENDELEA

Kifo chake, ufufuo na kupaa, havikuhitimisha huduma yake, bali ilitiwa moto na kuizidishwa ndani yetu! Hatujaunganishwa katika kifo na ufufuo wake tu, bali na kupaa kwake pia, 'Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho." Ef. 2:6. Mbegu ya ngano ilikuwa ya kulisha mataifa, haikubaki peke yake, bali ilianguka katika nchi na kufa, na kuzaa mazao mengi! Yohana 12:24. Kupambazuka kwa ukweli huu katika ufahamu wa mwamini utalibadilisha kanisa! Ekklesia wa Mungu ni sauti yake na kielelezo duniani! Jengo lake, watenda kazi wake, hekalu lake, makao yake, mfano wake, uwepo wake umejulikana na kusomwa na watu wote! Neno lake la asili lilifanyika mwili. Maisha ya kawaida kuwasiliana na nguvu ya ziada! John G Lake aliandika, "Ushindani wa karne umekuwa wa kuikomboa nafsi kutokana na tafsiri dhaifu. Bado ulimwengu unangoja kumwona Yesu kama alivyo; Yesu wa ajabu, Yesu mkuu, Yesu wa huruma, Yesu mwenye uwezo, Yesu wa ajabu katika vizazi vyote. Ondoa vifungo, mwache apate nafasi ya kuwabariki wanadamu kupitia wewe pasipo mipaka!" Mfanywe wapya katika roho ya nia zenu! Ef. 4:23. Paulo alisema haya katika 2Kor. 6:12, "Hamsongwi ndani yetu, bali mwasongwa katika mioyo yenu!" Na katika 1Kor. 4:8 anasema, "Mmekwisha kushiba, mmekwisha kupata utajiri, mmemiliki pasipo sisi ( sio mafundisho ya Paulo yaliyotufanya sisi kuwa vile tulivyo; ulikuwa ni utii wa Kristo); laiti mngemiliki, ili sisi nasi tumiliki pamoja nanyi!" Jinsi ilivyo fursa ya kutisha kutambua na kupendelewa

katika kweli iliyokuwako daima. "Siwaandikii amri mpya, ila amri ya zamani mliyokuwa nayo tangu mwanzo. Tena nawaandikia amri mpya, neno lililo kweli ndani yake na ndani yenu!" 1Yoh. 2:7,8.

### MLIPUKO WA HABARI!

"Wavuvi wawili wasioelimika wanamponya mtu aliyekuwa kiwete kwa zaidi ya miaka 40! Ulikuwa mguso wa ajabu ambao wanaume 5000 waliamini!" Mdo 4:13. Wakati wa Kanisa la kwanza hakukuwa na Biblia iliyokuwa imeandikwa kwa miongo kadhaa, na watu walio wengi hawakujua kusoma; hata hivyo Neno liliendelea na idadi ya wanafunzi ilizidishwa kwa nguvu. Mdo 6:7. Paulo anaona kwa uthibisho hatima ya Neno lililoandikwa si katika vibao vya mawe, au kuandikwa na kufasiriwa kwa matakwa ya mtu, wala kuhifadhiwa katika nakala milioni nyingi za Biblia na maktaba za maandiko, katika kila tafsiri na lugha; wala si katika matangazo ya redio za kikristo na televisheni; bali katika mfano na sura ya Mungu iliyochorwa kwa Roho wa Mungu katika vibao vya mioyo ya watu; wakiishi na kurudisha utukufu kama kwa kioo, thamani ile ile ya tabia ya Roho, ambayo ilionekana katika maisha ya Kristo; "Inajulikana na kusomwa na watu wote!" Oh! Ni umati wa aina gani, ni mguso wa aina gani! Ninapenda hivyo; wala si kuwachanganya makundi, bali kuwaunganisha! Nuru ya kweli inayomwangaza kila mtu imekuja. 2Kor. 3:2,3,18; Yoh. 1:9. "Bali kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu." 2Kor. 4:2. Juhudi zote za Kikristo kwa njia ya matangazo na miundo ya makanisa bila kujali ni watu kiasi gani tunahusika, zinaleta mguso kama wa mtu wa pili tu, ili kufikia kwenye cheo cha utimilifu wa Kristo!

Neno la milele, Neno lililokuwako tangu mwanzo, sasa pia limekuwa Neno la mwisho; mpango wote wa mawazo matakatifu ya Mungu, yakifikia upeo ndani ya mmoja ambaye ni Yesu, sasa umezidishwa pasipo kiasi, ili kumfunulia kila mtu alivyounganika kikamilifu katika ndoto ya upendo wa Mungu. Ebr. 1:1,2. Nabii Habakuki aliona kuwa ufunuo wa wenye haki kwa imani ungewasilishwa kwa uwazi sana, kiasi kwamba dunia ingejawa na maarifa ya utukufu wa Bwana, kama maji yaifunikavyo bahari. "Iandike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji." Hab. 2:2,4,14. Hakuna kitakachomhamasisha mtu binafsi zaidi kuliko kuelewa ukweli wa utambulisho wa Roho, kuhesabiwa haki kwake na kuunganishwa na Mungu. Haki ipatikanayo kwa imani sio namna mpya ya kukubaliana na taratibu za sheria, bali ni kioo kinachorudisha mwanga wa sura na mfano wa Mungu kama kwa kioo, akikombo na kujifunua katika mwanadamu. Mw. 1:26. "Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tuliloliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya Neno la uzima! Wapenzi, siwaandikii amri mpya, ila amri ya zamani mliyokuwa nayo tangu mwanzo...Tena nawaandikia amri mpya, Neno lililo kweli ndani yake na ndani yenu! ...Naye ametupa akili kwamba tumjue yeye aliye wa kweli, nasi tumo ndani yake yeye aliye wa kweli." Yoh. 1:1,2; 2:7,8; 5:20.

### MABADILIKO MAKUBWA NDANI YA KANISA

Rick Joyner, Mwalimu wa kinabii kutoka Charlotte, USA, anasema, *"Ninaona fagio la mageuzi ya ukristo wa kibiblia unakuja, ambao ni ufahamu mkuu wa ukristo kwa namna mbili, kwa ulimwengu na kwa Kanisa, vitabadilika."*

Kwa kweli mabadiliko makubwa yanakuja kwa maisha ya kanisa kama tunavyoyajua. Umati wa waamini wanapata udhihirisho mpya katika mazingira ya nyumba ndogo



kuliko jengo kubwa na ubinafsi (Daima ni uchawi na uasi!) Kwa hiyo, kinachohitaji mageuzi, hakipo katika nafasi ya kwanza, kiwango au maelezo ya muundo wa kanisa, bali ujumbe uliomo ndani! Yale yaliyomo katika msingi wa ufahamu wetu juu ya kazi ya Kristo, yasipochukuliwa kwa ufunuo uliochorwa na Roho; ujazano mkubwa katika kanisa la nyumbani, mara utageuka kuwa mzigo ambao unawasitisha na kuwapooza waamini kwa miaka mingi. Paulo anasema katika 1Kor. 5:6-8, 'Chachu kidogo huchachusha donge zima.' Katika jambo hili, anaelekeza kwa uwazi kabisa kuhusu desturi; tohara ambayo inawakilisha kujitoa na kuwa na utendaji binafsi, ili kutofautisha na kutoa sifa kwa mtu binafsi. Hata msisitizo ulio mdogo juu ya juhudi na kujitoa binafsi, unabatilisha imani ambayo neema inaifunua, na shukurani kufanyika ubatili.

Kitu chochote katika imani yetu, hata kikiwa kidogo na kisicho na maana, ambacho tutatakiwa kukifanya ili kupata upendeleo fulani kutoka kwa Mungu, kinabatilisha nguvu ya msalaba, na kuturudisha nyuma chini ya utendaji wa sheria. "Tukishindana na kujilinganisha sisi kwa sisi, hatuna akili!" 2Kor. 10:12.

Wakristo wengi hawana tatizo la ukweli wa kwamba Kristo anafunuliwa na kupokelewa kwa imani; bali tatizo linakuja kwa mwenendo ambao kwa urahisi sana huchafuliwa kwa mambo yote ya utendaji na misismko kana kwamba ni mlipuko wa sheria, kama vile majivuno, mashindano, hatia, hofu, shuku, hukumu ya dhamiri n.k. Utendaji wa aina yoyote usiovuviwa na ufunuo wa neema, unaleta matokeo ya matendo mafu! Ni mwenendo wa imani iliyovuviwa na kudumu inayoleta ushindi katika maisha! Gal. 3:2,3.

Imani inatiwa nguvu kwa thamani iliyofunuliwa (Gal. 5:6); Upendo unaona kuwa kuna jambo lililotokea kwa mwanadamu katika Kristo ambalo lina mamlaka na matokeo makubwa kuliko yaliyotokea kwa mwanadamu wakati wa anguko la Adamu. Rum. 5:14-21; 2Kor. 14-21. Pia ni bora zaidi kwa kivuli cha kiunabii kilichodumishwa na desturi, kama vile mtoto aliyezaliwa alivyo bora zaidi kuliko mfuko ambao ulitunza na kushikilia mbegu na mimba ya ahadi. Kol. 2:8,17; Gal. 4:1-10. Imani inatambua kuwa hitimisho la neema ni mwanadamu kuunganishwa katika Kristo.

#### MTAZAMO WA IMANI SAFI

Kamwe imani haijawa ya lazima, wala si nguvu ya kutoka nchi za nje, bali ni sauti ya kujulikana itafutayo mwitikio ndani ya mtu. "Basi imani ni *kuwa na hakika* ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Ebr. 11:1. Ikiwa imani ni kitu halisi na ushuhuda wa vitu visivyoonekana, basi tunatarajia kitu gani? Inakuwaje udhihirisho wowote wa ulinganifu wowote (au upungufu wake) unaongeza au kutoa thamani kwa kile ambacho imani tayari inakiona, inakijua na kukufurahia? Paulo anajifunza maana yake nini kuridhika katika sifa mbaya na sifa njema, katika kuwa na vitu vingi na kupungukiwa! Hili linatushauri kwamba, kuwa na vitu vingi daima sio dalili ya wema wa Mungu, wala kupungukiwa na vitu, kuwa ni dalili ya kukosekana kwa uwepo wa Mungu! Filipi 4:11,12; Hab. 3:17-19. Imani inaelewa kujaa tele; utimilifu wake unaendelea ndani yetu!

Roho ya imani ni zaidi sana kuliko kuwa 'kati ya nia mbili!' Sio daraja la akili kati ya vile usivyo navyo na vile unavyohitaji! Hali hiyo inaitwa fikira sahihi, au upangaji malengo mzuri, hali ambayo sisi sote tunajua kama sheria ya asili kama vile kupanda na kuvuna, ilivyo sheria ya asili pia. Hakuna ubaya wowote katika hilo; ni jinsi

ambavyo shughuli yoyote au mafanikio ya mtu binafsi hufanywa katika utendaji wa akili ya kawaida. Roho ya imani hufanya kazi katika kipimo cha maana iliyo kubwa zaidi. Kiini chake kimejengwa katika yale Mungu ayajuayo: Mungu anamwona mwanadamu akiwa ameunganishwa katika Kristo. "Mungu huyataja yale yasiyokuwako (yasiyoonekana) kana kwamba yamekuwako." Rum. 4:17. "Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani; kama ilivyoandikwa, 'Naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena,' sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena; wakati hatuviangalii vinavyoonekana, bali visivyonekana." 2Kor. 4:13,18. Tambua kwamba aina ya imani hii siyo iliyo kipofu, aina ya imani inayoruka-ruka gizani; bali inaona, na kwa hiyo hunena ukweli mkuu. "Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu (kupunguzwa mpaka ufahamu wa mwanadamu), bali yanayofundishwa na Roho, tukiyaifasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni." 1Kor. 2:13. "Kilindi chapiga kelele kwa kilindi!" Zab. 42:7. Paulo ana uhakika kabisa kuhusu ukweli kwamba mwanadamu ni roho, kwamba anakataa kuharibu Neno ili kulibana na kuliweka katika mfano dhaifu wa ufahamu wa kawaida, au mawazo ya mapokeo maarufu ya kibinadamu; bali kwa maelezo wazi (yalivyofunguliwa) ya kweli, wazo la Mungu lililofunuliwa katika sura ya Kristo, kama vile katika kioo, anaishuhudia kila dhamiri ya mtu. 2Kor. 3:18; 4:2. Anasema, "Kwa hayo, myasomapo mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo," Ef. 3:4. Mwanadamu amepangiwa kuishi katika maisha ya hali ya juu ya Neno iliyowashwa moto na kudumishwa kwa maelezo ya wazo la Mungu. (Kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu). Uhalisi wa imani hii unapatikana katika ufunuo wa utambulisho wa roho ya kweli. "Alituzaa sisi kwa Neno la kweli." Kuendelea katika Neno hili ni kugundua sheria ya kuwekwa huru na kuwa wana! Yak. 1:18,25; Yoh. 8:31,32,36. Katika siku hizi za mwisho Mungu amesema nasi katika Mwana! Ebr. 1:2. Imani hii inatoka kwa Mungu; ni imani ya Mungu. Yeye ni mwanzo na mwanzilishi, vile vile ni mwisho na utimifu wa imani yetu." War. 1:17; Ebr. 12:2. Inawezekanaje baba wa uongo kushindana na Baba wa milele na Baba wa kweli?

Uhalisi wa imani ya Simoni ulikuwa ni utambulisho wake wa roho, uwana wake wa kweli. "Simoni, mwana wa Yona, Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu." Imani ya Ibrahimu haikuweza kupata uhalisi wake katika Isaka kama sehemu ya kwanza, bali katika urafiki na Mungu, uliojengwa katika utambulisho wa roho yake! (Utambulisho wake umefunuliwa katika jina lake la imani, baba wa mataifa mengi!) Hapa kuna siri ya imani yake: "Mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana, asema Bwana!" Mw. 15:1,6. Imani ni 'urafiki na Mungu' kabla ya kitu chochote kingine! Jambo linalofanya urafiki na Mungu, sio tu kwamba linawezekana, bali pia halizuiliki, ni ufunuo wa mwanzo wa mwanadamu (utambulisho wa kweli wa roho) umehifadhiwa bila makosa. Kitu chochote, hata Isaka ni lazima aende madhabahuni kuliko kuwakilisha kitu halisi! Imani ya Ibrahimu ilihesabiwa kwake kuwa haki, miaka ishirini na tano kabla ya Isaka! Rum. 4. Imani hii ni zawadi inayopatikana sio kwa ushindi wa nidhamu ya kidini, kwa mfano: kusoma kwa bidii, kutafakari, kufunga, kutoa, maombi na maigizo ya ukiri, n.k. (si kwamba ni makosa kufanya nidhamu hizi, ikiwa ni kwa sababu ya, lakini sio ili iwe!) Ef. 2:8.

Neno hai la milele lilifunuliwa katika maisha, kifo na ufufuo wa Yesu kama uzima wa wanadamu; kifo na ufufuo huchochea ufunuo wa imani katika dhamiri ya mtu. Rum. 10:17. Hii ni siri ambayo ilifichwa kwa miaka mingi. "Ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wanalijua, wasingalimsulubisha Bwana wa utukufu." 1Kor. 2:7,8. Imani ya Mungu inafunua kusudi na wazo lake la milele, ambalo ni kuvijumlisha vitu vyote ndani yake, vitu vya mbinguni, na vitu vya duniani pia! Ef. 1:9,10; 3:11. Mungu alifanya kazi ya kutosha katika Kristo kuupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao! 2Kor. 5:19. "Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu! Rum. 8:19.

## UHALISI WA KWELI WA MWANADAMU NA HAKI VIMEFUNULIWA

Injili inafunua kuwa Mungu aliukomboza ulimwengu kwa njia ya utii wa Mwana. Je inaiacha wapi hatia ya ulimwengu kama ilivyoamriwa kwa njia ya sheria; au kutokuwa na hatia kunakofunuliwa katika Injili? "Hakika ameyachukua masikitiko yetu, amejitwika huzuni zetu; Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona." Is. 53:4,5. "Ikiwa mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi, kadhalika ina maana kuwa walikufa wote." (Kifo chake kilikuwa kifo chao) 2Kor. 5:14. Injili haihusu upendo wa Mungu kwa watu wazuri na tabia nzuri, bali inahusu mpango wa Mungu wa kupatanisha uadui wa mwanadamu na nafsi yake. "Kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi." Rum. 5:8. "Kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima." Rum. 5:18. (JB Phillips). Mafanikio ya ukombozi haupimwi kwa uwezo wa mtu wa kujibadilisha yeye mwenyewe, bali kwa tendo moja la Mungu la neema katika Kristo linatambuliwa. Injili inaeleza kuwa kuna jambo lilitokea kwa mwanadamu katika Kristo, lenye matokeo makubwa zaidi kuliko yale yaliyowatokea katika Adamu Rum. 5:14-21. *Katika maandishi haya, ni wazi kwamba Paulo anawaona watu wote, bila ubaguzi, wakipokea faida kubwa kutoka katika utume wa Kristo, kuliko walivyoteseka na maumivu yaliyotokana na anguko la Adamu. Kundi lile lile la watu walivyofanywa kuwa wenye dhambi kwa kutokutii kwa mmoja, wanafanywa wenye haki kwa utii wa mwingine.* (Tafsiri ya mwendelezo, kitabu cha Andre Rabe, Maajabu katika Kristo).

Mwanadamu alifanyika kiumbe kipya katika Kristo. (2Kor. 5:17; 'imekuwa na amekuwa' ni hitimisho na sio sharti! Tazama mistari 14-21; pia Rum. 8:31, "Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?" Injili inafunua ukweli kwamba Mungu yuko kwa ajili yetu!) "Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi." 1Kor. 1:30. "Hii ina maana kuwa ufahamu wetu na hukumu ya mwanadamu haviwezi tena kuwa msingi wa maisha yao ya nje." 2Kor. 5:16. Ushirika wa wanadamu katika Kristo tangu kabla ya msingi wa dunia, ndio msingi wa Mungu kushughulika na mwanadamu. Ef.1:4. Petro anasema, "Mungu amenionya, Nisimwite mtu awaye yote mchafu wala najisi. Mdo 10:15,28. Paulo anamwelekeza Tito kuwa, "Wasimtukane mtu yeyote, wasiwe wagomvi, wawe wema, wakionyesha upole wote kwa watu wote. Maana hapo zamani sisi nasi tulikuwa hatuna akili, tulikuwa waasi, tumedanganywa, huku tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na husuda, tukichukiza na kuchukiana." Tito 3:2,3. Kulingana na asili na uhalisi wetu wa kweli uliofunuliwa katika Neno la kweli. Yakobo katika sura ya 3:9 anasema kuwa, hatuwezi tena kumtukuza Mungu, na kwa ulimi uo huo kulaani na kuwahukumu wanadamu waliofanywa kwa mfano wa Mungu. Yesu alizungumzia kwa mifano kuhusu kondoo aliyepotea, shilingi iliyopotea na mwana mpotevu; kwa wazi kabisa anafunua kwamba, katika macho ya mmiliki wa asili, mwenye dhambi hajapata kupoteza thamani yake. Luka 15. "Alitatua tatizo la dhambi kwa wema, sio dhambi zetu tu, bali na za ulimwengu wote!" 1Yoh. 2:2.

Hiki ni kiini cha ukweli ambao ufahamu wake unamweka mtu huru, kuwa huru kweli kweli. Je, ulimwengu umesikia habari njema kweli kweli za kuachiliwa kwao, au bado mwanadamu ameshikilia utumwa kupitia Injili ya uongo, ambayo inawaacha makundi ama kutokujali au kuhukumikiwa? Yohana mbatizaji anamwonyesha Mwana-kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu; na ndipo anaendeleza mtindo wake wa zamani wa mahubiri na kumhukumu Herode. Badala ya kuwa ndiye mwanafunzi wa kwanza wa Yesu, ambaye hakuja kuuhukumu ulimwengu, anaendelea katika madhabahu yake mwenyewe, anawafundisha wanafunzi kuwa wageuke na kuacha

kuzoeana na Mafarisayo kuliko Yesu. "Tunafunga na kuomba, wakati ninyi mnakula na kunywa, ninyi ni walafi na walevi, rafiki wa watoza ushuru na makahaba!" Luka 5:33; Math. 9:14,16,17. Yohana akiwa gerezani anachukizwa na anahoji ukombozi, "Wewe ndiwe yule ajaye, au tutazamie wimbi lingine au uamsho mwingine?" Math. 11:3,6. Leo kuna wahubiri wengi wakaidi wanaochukua vikwazo vya Injili hii, na kukataa kujitoa kwenye haki inayotoka kwa Mungu, na kupendelea njia zao za zamani za kutafuta kuanzisha haki ya kuigiza kwa njia ya sheria ngumu na masharti; wakihubiri hukumu yenye msukumo na mfadhaiko uliosababishwa na kuwachanganya zaidi kuliko kuleta ufumbuzi. Kuna tofauti kubwa kati ya juhudi kwa ajili ya Mungu na juhudi ya Bwana. Haki kwa njia ya imani ndiyo inayowasha moto wa juhudi ya Bwana moyoni. Rum.10:1-4. Wenye dhambi walivutwa kwenda kwa Yesu, si kwa sababu alieleza kukubaliana na sheria, kama vile, "Unaweza kutenda dhambi bora usikamatwe, au jaribu kwa kufanya kidogo!" Bali ni kwa sababu alijifunua, na kwa upande wake waliona kuakisi kama kwa kioo asili yao ya kweli, uhalisi na bila hatia! Walitambua kuwa uongo walioushika kama ndio uhalisi wao, haukuwa na nguvu dhidi ya mlio wa dhamiri zao. Yesu hakumwambia kahaba, "Nenda ukatende dhambi kidogo," Alimwambia, "Nenda usitende dhambi tena!"

## UHAI WA KANISA

Maelezo yoyote ya kanisa tunayoweza kuyazoea ambayo hayafunui ukweli wa kufunguliwa kwa uwana wa asili wa mwanadamu, uhalisi wa roho na bila hatia, yatamwacha mtu bila ufanisi wala matunda, na yatashindwa kuwekeza uhai kwa ulimwengu. "Juu ya mwamba huu, nitalijenga kanisa langu." Ekklesia, linatafsiriwa kanisa, liko katika nafasi ya kwanza, mwitikio wa sauti ya kufanyika mwili, kufunua asili ya uhalisi wa mwanadamu, na kutangaza kutokuwa na hatia kwa mwanadamu. (*Gr. ecclesia, ek+kaleo*, kuita kwa jina). Yesu analielezea Neno katika mtiririko wa kufungua kuwa Mwana wa Adamu ni nani hasa; Mwana wa Adamu ni Mwana wa Mungu. Yeye ni Kristo, Mwokozi wa ulimwengu aliyepakwa mafuta! Hapa kuna swali kubwa ambalo kanisa linajibu: "Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?" Mwili na damu hushusha fikira za mtu kumleta katika mwili, "Simoni Bar-yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni!" Baba wa Yesu ni Baba wa kweli wa mwanadamu. Math. 16:13-19. Shetani ni baba wa uongo tu Yoh. 8:44. Kutokuamini kwa mwanadamu kunampa nguvu adui kuwapofusha akili zao katika ujinga. 2Kor. 4:4. Ekklesia hubeba funguo za ufalme na milango ya kuzimu haitashinda dhidi ya sauti ya kanisa. (*Gr. Kuzimu, hades, hutokana na ha+ideis*).

"Humkumbuki Mwamba aliyekuzaa, Mungu aliyekuzaa umemsahau." Mungu ni Baba wa milele! Hakuna chochote kitakachofuta ubaba wake wa asili yake! Is. 9:6,7. "Miisho yote ya dunia itakumbuka, na watu watamrejea Bwana." Zab. 22:27,30,31. Yeye ni Baba ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa. (utambulisho) Ef. 3:15. Kwa sababu tunashiriki asili moja, kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake. Ebr. 2:11. Mwanzo wetu halisi umehifadhiwa na kufunuliwa katika yeye! "Nisikilizeni, ninyi mnaoifuatia haki; ninyi mnaomtafuta Bwana; uangalieni mwamba ule ambao mlitolewa kwa kuchongwa, na tundu la shimo ambalo mlitolewa kwa kuchimbuliwa." Is. 51:1.

## SHERIA KAMILIFU YA UHURU

Uungu unaonekana na kufafanuliwa katika ubinadamu! Mw. 1:26; Kol. 2:9,10. Gen.1:26, Col.2:9,10. Ukishawishika kuhusu uhalisi wako wa kweli, unakutia nguvu kuwa na uadilifu wa hali ya juu; hili linakufanya kutenda mambo zaidi ya wajibu.

*Kutenda mema tu kwa sababu ni wajibu wa mtu ni vizuri; lakini tendo jema ambalo halitokani na sheria ya kuwajibika linapendeza zaidi kuliko lolote. Thomas Hardy.*

Katika Agano Jipya, Yakobo, ndugu mdogo wa Yesu, anaandika kuhusu wazo la nguvu na kuliita 'Sheria kamilifu iliyo ya uhuru.' Yak. 1:17,18,23-25. Sheria hii inatoa changamoto kiutendaji, namna ya kufikiri na kuhisi kuhusu wengine na sisi wenyewe. Yakobo anaongea kuhusu Neno la kweli linaloakisi sura ya uzao wa mtu (mwanzo) kama vile katika kioo. Neno linalomtangaza Mungu kuwa ndiye asili yetu ya kweli, analiita, sheria kamilifu ya uhuru. Sheria ya uhuru mkamilifu katika kigriki ni, *nomon teleion eleutherias*, yana maana ifuatayo: *nomon*, sheria, amri; *teleios*, timilifu au kamilifu; *eleutherias*, isiyozuilika, isiyosamehewa kutoka wajibu au madaraka. 'Hakuna uzito, yeye ni ndugu yangu' inakufanya kutenda zaidi ya wajibu pekee.

Kuwa mtendaji wa neno maana yake nini? Kuna tofauti kubwa kati ya kufanya ili, na kufanya kwa sababu ya. Yakobo anasema kuwa kila mmoja anaweza kulisikia Neno la kweli (ushuhuda wa kweli wa utambulisho wa roho yake), lakini ikiwa anayoyasikia hayabadili utendaji wake na mtindo wa maisha ya hiari mbali na kujichanganya, anajidanganya nafsi yake. Ikiwa Yakobo alikuwa anainua wajibu kimaadili tu ili kuwa na tabia njema, mchango wake ungekuwa nje ya mtiririko wa habari. Ndipo tungeweza pia kuendelea na juhudi zetu za kufanikiwa chini ya sheria ya Musa. Lakini Yakobo analiweka wazi kabisa kuhusu kutokutenda neno maana yake nini. Yule anayekwenda mbali na aliyoyasikia (neno la kweli, 1:17,18), ni yule ambaye anasahau mara moja kuwa yeye ni mtu wa namna gani.(22-24). Kwenda mbali maana yake kuanguka katika mfano wa utaratibu wa zamani wa kufikiri na kusema kuhusu wewe mwenyewe pamoja na wengine, kuvutwa mbali na Neno la kweli. Majaribu na upinzani vinapokuja, chombo kinakosa mwelekeo na kuchukuliwa na mawimbi na kupeperushwa na kuvunjika, kwa kuwa na nia mbili. Mtendaji wa Neno ni yule aonaye kwa mtazamo wa ndani ukweli kuhusu asili yake katika Mungu, kama msingi wa uhalisi wake wa kweli, na kwamba kila upinzani unabatilika. Utendaji wa neno ni tendo na mazungumzo yanayovuviwa na ukweli wa uhalisi wa roho ya mtu uliofunuliwa na kutambulika. Yak. 1:19,25; 3:2. Yesu naye anasema jambo lile lile kwamba, mtu asiposikia na na kuchimba kina ili kuweka msingi juu ya Mwamba, jengo alijengalo mtu huyo litaangushwa na dhoruba ya maisha. Luka 6:47-49.

## UTII WA IMANI DHIDI YA UTII WA SHERIA

Je kutenda na kutendewa kunatokana na sheria au kunatokana na imani? Wakristo wengi waaminifu pamoja na viongozi wao hawajui tofauti. Wanaweza kufundisha kujitolea, nidhamu na utii kwa shauku kubwa, lakini kukosa shabaha! Uhalali unaleta matokeo ya shuku, kukata tamaa, hatia, hukumu na kifo! Paulo anaifafanua huduma yake na utume katika Rum. 1:5, "Ambaye katika yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani, kwa ajili ya jina lake." Analiona kila taifa limejumlishwa katika ufunuo wa neema. Katika Ef. 3:9-11, analiweka namna hii, "Kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote. Ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu

Bwana wetu. "Yale ambayo Mungu aliweza kuwasiliana katika Kristo, sasa yanaonekana katika mwanadamu, ili kuwasiliana katika milki ya roho. Siri ni "Kristo ndani yenu" Kol. 1:25-27. Tabia ya kusukumwa na sheria inapunguza mguso wa maisha yako kwa milki ya kawaida; wakati ukweli wa imani una mguso wa haraka katika milki ya roho.

Neno la kigriki juu ya utii, *upo+akoo*, lina maana ya kuwa chini ya nguvu ya msukumo wa kusikia. Paulo anaelewa kuwa kusikia kunaleta imani. Rum. 10:17. Katika Mdo 14:1 Luka anasema, "Paulo alihubiri kiasi kwamba watu wengi waliamini." Tendo lolote linalosukumwa na hatia, kujiona duni au batili, vile vile litaleta matokeo ya hatia, kujiona duni na ubatili.

Kuchimba zaidi ardhi ili kujenga msingi wako juu ya Mwamba, au kama Yakobo anavyosema, "Aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru," linajumlishwa katika 2Kor. 13:5,8; "Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Maana hatuwezi kutenda neno lolote kinyume cha kweli, bali kwa ajili ya kweli!" Elewa kwamba ombi sio kujichunguza mwenendo bali imani! Agano Jipya halifunui jambo jipya, sheria zilizotengenezwa upya ili kukubaliana na amri kumi; bali ni ufunuo wa uhalisi wa mwanadamu uliokombolewa!

Injili ni 'kuona kwanza' kabla ya 'kutenda,' hata kufa kwako si kutenda, ni kuona kwamba umekufa katika kifo chake; hakika alikufa kifo chako! Rum. 6:11; 1Kor. 1:30. Nguvu nyingi sana za kidini zinapotezwa juu ya majaribio yasiyofaa, kufanya mambo ambayo tayari yalifanywa; kufanya vile ambavyo tayari ndivyo ulivyo! Kwa sababu ya ujinga, ukristo umekuwa kama Wabuddha; watu wamejiingiza kikamilifu katika hali ya kutokuzaa matunda, bali juhudi za kuendelea kufa wenyewe.

Sheria ya neema ni sawa na sheria ya imani; ni sheria ya ushirika au sheria ya utambulisho. Pia Paulo anaita sheria ya roho wa uzima katika Kristo Yesu. Rum. 8:1-4. Imani inamwunganisha mwanadamu kwenye ukweli mkuu kuliko kile ambacho ni wajibu wake wa thawabu au adhabu tu. 'Sasa, kwa mtu ambaye anafanya kazi, mshahara wake hauhesabiwi kuwa zawadi, bali ni wajibu wake.' Rum.4:4. Sheria ya utambulisho inafunua kuwa yaliyotokea kwa Yesu, wakati uo huo yalitokea kwa mwanadamu." Mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi walikufa wote." Tulishirikishwa ndani yake kabla ya msingi wa ulimwengu! Ef. 1:4. Tulisulibishwa pamoja naye, na kufufuka pamoja naye; Alijeruhiwa kwa ajili ya makosa yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.

Hili linaeleza jinsi tunavyoweza kushinda bila kushindana; jinsi tunavyoweza kushinda bila kuingia katika uwanja wa vita; Jinsi tunavyoweza kupata mavuno ambayo hatukuyatendea kazi, na jinsi ya kuacha kutokana na kutegemea kazi zetu! 1Kor. 9:24-27; Kut. 14:13,14; Zab. 44:3. "Mnasema bado miezi minne ndipo yaja mavuno; na mavuno yataleta chakula zaidi; zaidi ya kile kisichotosheleza. Yesu ana mavuno akilini mwake kwa ajili yetu, yale tusiyoyasumbukia! Mavuno ya juhudi zetu wenyewe na kazi, daima yanakatisha tamaa; mwanadamu hakukusudiwa kuishi kwa mkate tu. Hitaji la mwisho la mwanadamu ni kwa ajili ya kitu cha zaidi kuliko kile ambacho kwa hisia tu, wakati roho yake inaachwa kwa njaa.

## KILA NENO LITOKALO KATIKA KINYWA CHA MUNGU

Tumekusudiwa kuishi kwa udhihirisho wa asili ya wazo la Mungu kwetu. Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, ni jicho la chemchemi, wazo la mkono wa kwanza la asili, kuwa na tofauti kali dhidi ya wazo la aina ya mkono wa pili, lililopunguzwa nguvu kwa desturi na fasiri au tafsiri maarufu. Neno lililokuwako tangu mwanzo, ni chemchemi ya asili, wazo kamili la Mungu. Paulo anasema, "Lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo; bali kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu." 2Kor. 4:2.

Nia mpya ni tunda la roho; ni ufunuo wala sio juhudi ya kusoma sana. Huwezi kugeuza nia yako kuwa mpya, lakini unaweza kugeuzwa ndani ya roho yako. "Kumtazama katika kioo, ndipo tunageuzwa kufanana naye." Kumtazama kwa njia nyingine yoyote hakuleti badiliko lolote, bali hatia zaidi, kujiona duni na hukumu. Hakuna kiletacho mguso wa mwendelezo wa wazo na kutulia kwa nia zaidi kuliko ifanyavyo kweli. Kweli inalia ndani ya kila dhamiri ya mtu.

Isaya anasema kuwa waliochoka na kumngoja Bwana watapata nguvu mpya (sio kwamba wataendelea kufanya waliyozoea kufanya, bali kwamba waweze kuingia katika kipimo kipa cha maisha), watapanda juu kwa mbawa kama tai! Kuna matazamio mapya yanangojewa kwa wale ambao huungana na mawazo ya Mungu. Neno la Kiebrania *kawva*, linatafsiriwa, kungojea, likiwa na maana ya kuunganishwa au kushikanishwa pamoja; kama vile nyaya mbili zinavyoviringwa pamoja ili kuzidisha nguvu yake! Jambo hili si uchaguzi wa kujifurahisha; ndiyo maisha yetu na mwenendo wa kila siku! Dini humpunguza Mungu kuwa kama mtu anayefaa: "Unapokuwa na shida ndipo unamfuta-futa Mungu na kumwita!" Unatakiwa kutambua kuwa ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu! Kuingia katika raha yake ni kutembea katika nuru, kuona yale Mungu anayoyaona, kusema yale anayoyasema! Wazo lake la milele linakuwa ndio kutafakari kwetu na mazungumzo yetu!

Neno la kwanza lilikuwa "Iwe nuru"- kukawa na nuru. Kwa hiyo neno lilikuwa "kuwe na!" Hapakuwa na neno lenye nguvu ya kushindana ili kupata kitu. "Mungu yule yule aliyesema, 'Nuru iangaze katika giza!' ameiwasha nuru ndani ya mioyo yetu, ambayo kuwaka kwake ni kuutambulisha utukufu wake (wazo), kama alivyoifunua katika sura ya Yesu Kristo." 2Kor. 4:6. *Knox*.

Mungu ametutunzia urithi usioharibika, usio na uchafu, na usiochakaa, mbali na mabishano yote.

"Mmekwisha kushiba, mmekwisha kupata utajiri, mmiliki pasipo sisi. Naam, laiti mngemiliki, ili sisi nasi tumiliki pamoja nanyi!" 1Kor. 4:8.

Macho ya ufahamu wetu yamemulikiwa kuujuu ukuu usiopimika wa nguvu zake ndani yetu tuaminio, sawasawa na utendaji wa uweza wake alioutenda katika Kristo, alipomfufua kutoka wafu na kumketisha mkono wake wa kuume, katika ulimwengu wa roho, juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo (Nguvu yake inakwenda juu ya kiwango cha kawaida). Hakuna mamlaka yenye ufafanuzi wowote, unaoweza kulinganishwa au kupingana na nafasi yake. Ef. 1:17-21. Kwa ajili ya habari njema: Tulipokuwa tungali katika dhambi, tukiwa tumekufa katika makosa yetu, alitufanya hai pamoja na Kristo (hii ndiyo maana ya neema: kuna jambo lilitokea kwa mwanadamu wakati alipofanywa hai!!!) Alitufufua pamoja naye, na kutuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, ndani ya Kristo

Yesu; ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu! Ef. 2:5-7.

Kukumbatia kipawa ni kutawala katika uzima Rum. 5:17. Kuamshwa kwa roho yako kumeandikwa katika kipimo cha Mungu. Ukweli uliotambuliwa unahimiza utawala wa roho. Kwa kuwa umefufuliwa pamoja na Kristo, zishughulishe akili zako na kweli za chumba cha kiti cha enzi. Kol. 3:1-16.

## MAJARIBU

Majaribu yanakuwa ni majaribu tu pale imani yako (utambulisho wa roho) inapotiwa changamoto, na kupokea utambulisho ulio duni. Yesu alifunga kwa siku arobaini; alipokuwa na njaa (mahitaji ya asili) Mara adui alitua changamoto utambulisho wake wa roho, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu!" Aliketi kisimani akiwa amechoka, ana njaa na kiu, lakini hivyo havikumshusha na kusahau kuwa yeye alikuwa ni wa namna gani. "Kama ungelijua mimi ni nani!" Yoh. 4. Mungu hajaribiwi; Hana kazi ya utani, wala hafanyii majaribio kusudi lake kwetu! Yak. 1:13. Mungu hawezi kuwa mwanzilishi wa nuru na giza wakati mmoja. Kila jaribu ni jaribio la giza ili kuizuia nuru. Kila kilicho chema na kikamilifu hushuka kutoka juu (iwapo ni chema, hakiwezi kuwa kibaya kwa wakati uo huo, iwapo ni kikamilifu hakiwezi kuthibitishwa na mtu; iwapo ni kipawa, hakiwezi kupatikana kwa kazi!) Baba wa mianga ndiye chanzo cha kipawa hiki cha ukamilifu; kwake yeye hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka. Mungu hawezi kubadilika katika tabia yake; hawezi kujikana mwenyewe. Maisha aliyoishi Yesu hakukubaliana wala kujichanganya kinyume na Baba wa mianga. Yeye ni nuru ya kweli inayomwangaza kila mtu. Sheria kamilifu ya uhuru, inakubaliana na neno la kweli, sura ya asili ya mwanadamu, inayoakisiwa kama kwa kioo katika Kristo. Yak. 1:17.

Kuuhesabu upinzani kuwa furaha kamili hakuleti maana yoyote kulingana na kweli ambayo hakuna kiwezacho kuipunguza! "Mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watamilifu bila kupungukiwa na neno." Yak. 1:2-4. Furaha si jambo fulani tufanyalo; ni matokeo ya lile tulijualo! "Kwa kuwa katika utamilifu wake sisi sote tulipokea" (Yoh. 1:16), "Nasi tumekamilika katika yeye." Ndani yake tunatambua ukamilifu wetu. Kol. 2:10. Haya ni maelezo ambayo hayawezi kuwa ni ya makisio tu. Kujua uadilifu wa kujulikana kwako ni ufunguo wa kushinda majaribu. Jaribu linataka kukushawishi kuwa dhaifu, mpungufu na asiyekamilika. Hekima itokayo juu inakuthibitishia utamilifu na ukamilifu. Saburi ni zaidi ya uvumilivu katika mbio; ni mazingira ya ushindi yanayolinda ushawishi wa imani kwa furaha. "Maana walipokuwa wakijaribiwa kwa dhiki nyingi, wingi wa furaha yao na umaskini wao uliokuwa mwingi uliwaongezea utajiri wa ukarimu wao." 2Kor. 8:2. Kutoa kwao kulikuwa kielelezo cha kuona, kufanya na kwenda zaidi ya sheria ya desturi ya sehemu ya kumi. Badala ya hasira, fadhaa na aibu sasa upinzani unawaletea furaha isiyonenea! Petro anaongea kuhusu furaha inayobubujika ndani yako kama chemchemi ya kisima. 1Pet. 1:6-8. Yakobo anatomia neno *hegeomai* katika Yak. 1:2, lililo na maana ya kuonesha furaha katika eneo maalumu la mamlaka! Furaha ni nguvu ya kutawala inayofukuza hofu, fadhaa, huzuni na hasira! Haki ipatikanayo kwa imani hufurahi mambo yanapokwenda vibaya! Hab. 2:4; 3:17-19. Miguu ya nyuma huteleza katika njia kuu ya hatari! Kuishi bila kukata tamaa ni ushuhuda wa Paulo katika Warumi 5:3-5. "Mkakubali kwa furaha kunyang'anywa mali zenu" kunaonesha kuwa katika tofauti kubwa ya kujiuliza, mpaka mtu atakapogundua nafasi ya ukamilifu ambayo haiwezi kuingiliwa na kitu kingine! "Kwa maana mlukufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu." Ebr. 10:34; Wafil. 4:12; Kol. 3:3.



Kila linapotokea jaribu katika akili zetu, kusudi lake ni kuipata sauti yetu ili kuipata kura yetu pia. Lengo lake ni kutushawishi kukubali kuwa dai lake halizuiliki. Shauku yake ni kupofusha akili zetu kutoka hali ya ukweli wa kiroho ili kwamba ile iliyo haki yetu katika Kristo, na kujua kuwa sisi ni nani katika yeye, kuonekane kutoeleweka na kutokufaa! (*Gr. exelko*, kushawishi kwa mfano wa kuwinda au kuvua; na *deleatzo* kutokana na neno *dolos*, kudanganya kwa chambo). Yak. 1:14. Tamaa inapochukua mimba, inafanyika kuwa mzazi wa dhambi. "Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika!" Yak. 1:19. Kushikamana na jaribu, kukubaliana au kulitambua, kunaiwasha sumu yake, ndipo unakuwa ugonjwa, dhambi na kukatisha tamaa au kuleta mfidhaiko! Moja ya uongo mkubwa wa upinzani ambao unaweza kukuangusha, ni wazo la kwamba unapitia katika hali ngumu ambayo haina namna ya kutoka humo. "Hakuna jaribu lililo maalumu kwa mwanadamu ambalo huwezi kulipinga. Mungu ametupa njia ya kuepuka, siyo ya kukimbia, bali kukabiliana nalo na kushinda kwa uthibitisho kamili na kukubalika kwa ushindi wa Kristo kwa niaba yetu. 1Kor. 10:13. Sauti ya imani ya furaha ni ukabiliano wa nguvu kwa upinzani. Tunatenda katika roho kinyume cha hali halisi inavyodai. "Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi." 2Tim. 1:7. "Basi mtiini Mungu, mpingeni Shetani, naye atawakimbia!" Yak. 4:7. Angalia ni nani anayekimbia, na anamkimbia nani! "Atawakimbia!" Hatujaitwa kukimbia na kujificha, bali kuamka na kuangaza! Kumtii Mungu ni siri ya kushinda majaribu. (*Gr. upotasso*, kutii, kunaonyesha makubaliano ya sisi kwa sisi); kushikamana na Mungu katika mazungumzo yako, kwa sababu katika mguso wako wa ndani umethibitika katika kweli na ukamilifu. Uhalisi wa mguso wako utachochea mazungumzo yako; maneno yako yanakuwa ya mbinu na nguvu kwa vita. Is. 36:5. Daima nuru hupambana na kuifukuza giza. Kama pasingekuwa na adui, pasingekuwa na haja ya kujilinda; hata hivyo hatukuitwa kuwa na maisha ya mapambano na vita visivyokoma. Shikilia kweli ya utambulisho wa roho uliofunuliwa katika Kristo; huu ni mwanya katika Mwamba unaokuhifadhi kutokana na mawimbi na dhoruba; pia ni silaha yako ya vita. Ufunuo wa utii wa Kristo ni mkuki wenye makali, kwa huo tunateka kila fikira na kuvunja kila ngome 2Kor. 10:4,5. KJV au KJV Mpya. Kuijua kweli ni kumshinda adui aliyeshindwa. Kinga ya virusi katika mwili wako ni mfano mzuri wa matokeo ya chujio la Neno la kweli. Haitokei dhambi yoyote wala uovu ambao utapona kuchujwa kutokana na usalama ambao ni matokeo ya utii wake katika ukiri wako na dhamiri. Ebr. 10:1-3,19-25.

"Yeye astahimiliye majaribu ataipokea taji ya uzima." Yak. 1:12. Neno la kigriki kwa taji ni *stephanos*, lenye maana ya alama ya cheo cha kifalme, au shada la maua, iliyotolewa kama tuzo kwa washindi katika michezo. Lakini Mungu uzima kuwa ni kipawa, wala sio tuzo. Yak. 1:17. Hata hivyo, tuzo yetu ni kipawa, kwa sababu kuvumilia na saburi sio vitu tunavyovipata kwa juhudi na nguvu zetu, bali ni nguvu inayowaka ndani yetu kwa ufunuo wa Neno la kweli. Sisi ni tunda na ukumbusho wa uchungu wa nafsi yake. "Utimizezi wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka, kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema." Filipii 2:12,13.

Hatujaitwa kubishana, kujadiliana kwa kulinda mafundisho yetu, bali tumetiwa mafuta kumfurahia na kumdhahirisha Mungu!

## KUCHAGUA KANISA

Ukiyafikiria makanisa mbalimbali 30 mpaka 40 yanayoizunguka jamii yako, ni lipi ambalo wewe umetii na kujiweka chini ya mamlaka yake? Ni nani unayeshindana

naye, kumvumilia, kujitenga mbali naye, au kushirikiana naye? Ukweli uko pale pale kwamba, kuna kanisa MOJA tu! Hilo linaufanya uchaguzi kutokuwa na maana!

Umoja katika mwili wake kamwe hauwezi kulazimishwa kwa njia ya makubaliano au maafikiano. Umoja unapokelewa sawa na uponyaji au hali nyingine yoyote iliyomo katika ukombozi; ni kuachilia kitu ambacho tayari kilitokea Mungu alipoupatanisha ulimwengu na nafsi yake katika Kristo. Hili lilitokea tulipokuwa tungali maadui na wenye dhambi. Mungu aliukomesha uadui, kuwa mbali naye, matengano, dhambi na magonjwa. Kweli na nguvu ya Injili, daima hufunua jambo ambalo tayari lilitokea katika roho. Injili hii hutangazwa kwa mguso na ujasiri mkubwa. "Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani." Rum. 1:16,17. "Kwa kuwa tuna huduma hii, kwa jinsi tulivyopokea rehema, hatulegei; lakini tumekataa mambo ya aibu wala kuichanganya Injili na uongo kwa sababu ya yale tuyaonayo katika mwili. Hatuyaangalii yanayoonekana, bali yasiyoonekana! Tuna roho ile ile ya imani kama ilivyoandikwa, 'Naliamini na kwa sababu hiyo nalinena;' sisi nasi twaamini, na kwa sababu hiyo twanena." 2Kor. 4:1,2,13,18. Imani ni kukubaliana na Mungu, ni kuenenda katika nuru kama yeye alivyo katika nuru. Imani ni neema ya kuona ukombozi na maana yake, bila kuondoka katika mtazamo wa Mungu! Imani huona kuwa mavuno yameiva tayari! Mbegu ndani ya tunda tayari inatoka katika gamba la mbegu iliyopandwa! "Mungu huyataja mambo yasiyokuwapo kana kwamba yamekuwako!" Katika nuru yake tunaiona nuru, ndipo sasa tunaweza kuwa na nia moja na kunena lugha moja! Nuru yake hufanyiza hatua! Upendo wa Kristo unatubidisha, tunavutwa kuhusu wanadamu, tunamwona kila mmoja amejumlishwa, kutakaswa na kurejeshwa katika utimilifu wa uzima kwa njia ya utii na ushindi wa Kristo! Nuru ya Mungu inaunganisha! Fikiria za mwanadamu, mafundisho yake na desturi hugawanya. Kundi lolote au taasisi inayotenganika au kutawanyika mbali na kweli ya Injili ambayo ni hitimisho la mwanadamu katika Kristo, wanajidanganya na kubatilisha kile walichokipokea ndani yao.

Ekklesia analolijenga na kulifunua, kamwe halitishwi na maelezo mabaya au fikira na mitazamo mbalimbali. Kwa njia ya mvuto wa ufunuo wa tabia yake ndani yetu, kwa njia yetu anaishuhudia kila dhamiri ya mtu! Sisi ni barua hai, hati za uthibitisho, kufanyika mwili na kusudi lake la Mungu la milele linatangazwa kupitia maisha yetu, ili kujulikana na kusomwa na watu wote! 2Kor. 3:2,3,18. Milango ya kuzimu haitalishinda na kufanikiwa kuwafunga na kuwapofusha watu wasiione nuru yetu inayoangaza! Wafalme na viongozi watakutwa bila kizuizi kama kwa sumaku, kwenye ufunuo wa mfano wake, kusudi la kuwepo kwake katika mwili. Is. 60:1-3. Maisha yako ni mpango wa Mungu na ujumbe wa tumaini kwa dunia iliyokata tamaa. Yesu alisema, "Wapeni ninyi chakula! Wakamwambia, Tunawezaje kulisha makutano haya? Akawauliza, Mnayo mikate mingapi?" Marko 6:35-44.

"Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja." 1Kor. 1:10. Ikiwa Mungu anasema vile vile kama alivyosema katika Kristo kwa ulimwengu, akiwa ndani yetu, tunaweza kufanikiwa kusema vile vile kwa watu, kuhusu watu na sisi kwa sisi. Kuna ukweli mmoja tu, nuru moja, chemchemi moja, imani moja, msingi mmoja, Roho mmoja, Kichwa kimoja, mwili mmoja, Hekalu moja, Baba mmoja, naye ni wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote! Ef. 4:3-6. Hana patakatifu pengine anapopatamani kuwa makao yake, bali mwili wa mwanadamu. Utu wako kwake sio gereza, bali ni mahali maalumu! Hakuna mahali pa dhahabu panapofanyika au kumfunua zaidi! Umeufanyizwa kama fundi wa kushona! Unamtosha Mungu kama vile mipira ya mikono! Upendo wetu na heshima kwa ndugu

zetu vinafanana na upendo wetu, ibada na heshima kwa Muumba. Yak. 3:9; 1Yoh. 4:19,20; Gal. 5:14.

Ujinga, hofu na uadui, vimetutenga kwa karne nyingi na kutuibia umoja wa sisi kwa sisi. Sasa tumeitwa ili kutambuana! Kila ukuta wa matengano umevunjwa! Ef. 2:14,15; Filem. 6; Tit. 3:2; Gal. 3:28; Col. 3:11. Hakuna jina la alama au chapa linaloweza kukutofautisha zaidi au kukupa maisha yako ufafanuzi au mvuto zaidi kuliko Baba ambaye kutoka kwake kila jamaa, mbinguni na duniani hutajwa. Maisha yetu husherehekea ukweli kwamba Mungu aliupatanisha ulimwengu na nafsi yake. Aliukomesha uadui. Tumedhaminiwa na ujumbe wa kuleta amani duniani! Vita vimekwisha! Changamoto, "Kuwapenda adui zenu, na kuwatendea mema wote wanaowachukia na kuwanenea mabaya" sio suala la nadharia tena; bali ni uhalisi wa maisha yetu! Tunaelewa kuwa, "Vita vyetu SIO katika damu na nyama" maana yake ni kwamba hatuwezi kumlenga ndugu yetu tena! Mungu ni rafiki wa mwanadamu, na wala sio adui yake. Dalili za kutokukamilika; dhambi au magonjwa ndani ya mtu, havimfanyi kuwa adui.

Mazungumzo yetu yanathibitisha mvuto wetu. Mungu alitoa neema yake juu yetu, na upendo wake umemwagwa katika mioyo yetu; hatuna udhuru na kuhisi tofauti kati ya watu tena. Mwanadamu ni ndoto ya upendo wa Mungu.

Pia, hatuhitaji tena kubadili sheria ya uhuru kwa taratibu za sheria! Ushirika hausukumwi kwa nguvu!

## URAHISI WA INJILI

Paulo anaitikia katika hofu kwa waamini wa Galatia, akiwaonya kutokuipunguza nguvu ya Injili kwa taratibu za kibinadamu na amri za kidini kwamba zinatakiwa kuwa mchango wa mwili, kana kwamba yaliyotokea kwa mwanadamu katika Kristo hayakutosha. Tamko lolote ambalo bado mwanadamu anatakiwa kufanya ili kumpa sifa ya kukubalika, kupendwa au kupokea chochote kutoka kwa Mungu ni kama tusi la kuutukana msalabani. Si kwamba Mungu amekwazwa, bali linamwacha mtu akiwa amebatilika na kuchanganyikiwa.

Tuzo ndogo ya dhamiri hubatilisha kipawa! Matokeo yake ni kama chachu ichachushayo donge zima! Hata karama za Roho ni sawa na karama nyingine yoyote; haiwezi kupatikana kwa kazi. Sio tuzo ya juhudi ya kiroho au mafanikio; bila upendeleo, inaweza kupatikana kwa imani na shukurani tu! Chochote uwezacho kukipata kwa kazi, unaweza kukinunua pia! Unawezaje kununua kwa thamani inayopotea kitu ambacho tayari kilinunuliwa kwa damu ya uzima wa mwana-kondoo wa Mungu? Ni kama kujaribu kununua hazina isiyo na thamani, kwa fedha inayomilikiwa.

Kila hali ya ukristo wa kweli, pamoja na viwango vyote vya ukuaji wa kiroho na uzoefu, vimezungumzwa katika neno la mwisho kwa mwanadamu, na vinapokelewa kwa imani. Yesu katika ubinadamu wake ni kielelezo kamili na mfano halisi wa Mungu asiyeonekana aliyejifunua katika mwili wa kibinadamu. Yeye ni nuru inayoakisiwa kama kwa kioo kwa kila mtu. Anatangaza uwana wa kweli wa mwanadamu; Mwana wa Adamu yuko katika kweli, ni Mwana wa Mungu. Je, inawezekanaje baba wa uongo ashindane na kweli hiyo? Bila shaka wenye dhambi walivutwa bila kizuizi kwenda kwa Yesu! Ukweli wa ufunuo huu, ndio ukweli pekee unaompa mtu uhuru; Neno la neema ni chemchemi ya imani. "Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa Neno la Kristo." Rum. 10:17.

Tafsiri ya Kilatini iliyotokana na Kigriki imeelezea uongo kuhusu toba, ambayo imewafanya makundi ya waamini kukaa katika giza na utumwa kwa karne nyingi. Neno, *metanoia*, lenye maana ya mbadiliko wa asili wa nia, limetafsiriwa kimakosa kuwa toba! Dini imepalilia na tena kutiwa moyo na kuinyonyesha maziwa dhamiri ya dhambi kwa miaka mingi! Injili inafunua msingi wa kutokuwa na hatia kwa mtu. Kuitangaza Injili maana yake ni kutangaza kutokuwa na hatia kwa mwanadamu! Nuru ya Neno la milele la uzima la kweli, lilifunuliwa kwa mwanadamu katika Kristo, kama vile katika kioo, linatoa ufafanuzi wa mwisho na hitimisho kwa wokovu wa mwanadamu, uponyaji na uhusiano uliorejeshwa.

“Mungu hutaja mambo yasiyokuwako kana kwamba yamekuwapo!” Hii ni siri; milele imekuwa katika wakati uliopita! “Alijeruhiwa kwa makosa ya wanadamu, na kuchubuliwa kwa uovu wa mwanadamu. Kwa kupigwa kwake kizazi cha mwanadamu kiliponywa.” Tunasoma katika kitabu cha Waebrania kuwa katika Kristo, mpango wa asili wa mwanadamu ulionyeshwa; Yesu haoni haya kutuita sisi ndugu zake. Alitutakasa ili kufunua asili yetu ya kawaida! Mwanadamu amehifadhiwa katika nafasi ya kumiliki; kila kitu kinamtii yeye. Kutokuona kila kitu kikimtii mwanadamu mara, hakumfanyi Mungu kuwa mwongo; kwa wazi tunamwona Yesu kuwa ni mshindi. Rum. 3:3,4; Ebr. 2:8,9. Anamwonyesha mwanadamu kama kwa kioo! Kwa sababu hii, tunatangaza Injili kwa bidii na ushawishi; tukiishuhudia kila dhamiri ya mtu, tunamwomba kila mwanadamu kuiamini kweli ya Habari Njema kuhusu maisha yao. Hakuna msingi mwingine wa imani, au badiliko la kudumu! Tunapojiangalia na kumtazama pasipo kuvutwa na mengine, KAMA KWA KIOO, tunabadilishwa tufanane naye. “Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo.” 2Kor. 3:18. Ni katika kuugundua ukweli kuhusu sisi wenyewe, kama ilivyofunuliwa katika Kristo, kwamba imani inatuhimiza. Ef. 4:21-24. Hakuna mtazamo mwingine unaoweza kuleta badiliko la kweli, hata kwa tatizo lililo dogo kufikiriwa katika historia. Tatizo na dhambi ya dhamiri huleta hatia na kushindwa. Nuru huzaa nuru! “Paulo alihubiri KWA NAMNA AMBAYO wengi waliamini!” Mdo 14:1,9.

Hakuna maelezo mengine ya kufanyiza au jaribio la kubadili mwenendo, tabia, dalili za magonjwa au huzuni, namna ya mawazo, mazingira au uhusiano, yanayoweza kulinganishwa au kushindanishwa na wokovu kama ulivyofunuliwa katika Injili. Ni nguvu ya Mungu itendayo kazi ndani ya mtu! Mtu anapotakiwa kwanza kungojea dalili za magonjwa zitoweke kabla imani haijaanza na kumkiri Yesu, ni upumbavu! Hayo yataifanya imani, wokovu na uponyaji kuwa si vya lazima, si hivyo tu, bali kutokufaa pia.

Nje ya Injili hii shauri la mwanadamu huonekana kutokuwa na tumaini! Bali Habari Njema hufunua kuwa, KUNA JAMBO LIMETOKEA KWA MWANADAMU YESU ALIPOKUFA, ALIKWENDA KUZIMU, NA ALIFUFUKA, NA ALIPAA KWENDA KATIKA ENZI! Ikiwa mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi inawezekana kuwa na maana ya wote walikufa kweli! Kwa hiyo, tangu sasa na kuendelea haiwezekani kumtambua mtu yeyote kwa jinsi ya mwili! 2Kor.5:14-21. Namna tulivyojijua wenyewe pamoja na watu wengine hapo kwanza, sasa ni zaidi kwa uhalisi mkubwa. “Tukiupokea ushuhuda wa wanadamu, ushuhuda wa Mungu ni mkuu zaidi!” 1Yoh. 5:9. Mungu anamwonyesha Petro katika njia ya asili kabisa kwamba, kulingana na kazi aliyoikamilisha Yesu kwa niaba ya mwanadamu, mtu yeyote asiitwe mchafu wala najisi! Mdo 10:15,,28. Mungu alimtangaza mtu kuwa safi, aliyekombolewa, aliyeponywa na kurejeshwa! Paulo anamtia moyo Tito kutokumnenea mtu yeyote mabaya, bali aonyeshe upole wote kwa watu wote! Tit. 3:2-4. Yesu hakufa kwa ajili ya waamini peke yao; alitwaa huzuni, magonjwa na dhambi ya vizazi vyote juu yake. Huu ni uhalisi kabisa na mchanganyiko wa Injili ya neema, inayoleta imani ambayo ni

bayana! Kuyaelewa haya ndiko kunampa mtu imani. Mtu hawezi kutambuliwa kwa njia nyingine yoyote tena! Si mtazamo wa kujifurahisha au uchaguzi; sio kwa elimu ya juu ya mtu, mafundisho au hadithi zilizotungwa kwa wervevu! Hii ni Injili kama Mungu aionavyo na kuifunua katika Kristo na Maandiko!

Ustahiki wa kweli wa Injili umeanzishwa katika utii wa Kristo, na hauna uhusiano wowote na historia ya dalili au kiasi cha giza. Ili kuchunguza na kutafiti tatizo kwa bidii, ni kuvutwa kwenda mbali na msalaba. "Nili azimu nisijue neno lolote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa!" Lililotokea kwa mwanadamu pale msalabani, ndilo liliopo sasa! "

Roho Mtakatifu anatoa hukumu kwa ulimwengu ulio na dhambi moja tu, ya kumdharau Kristo. Dhambi nyingine yoyote imeshughulikiwa katika kifo chake. Pia anatoa hukumu kwa ulimwengu kuhusu haki, kwa sababu Yesu alikwenda kukaa pamoja na Baba. Yoh. 16:7-11. Hakuuacha ulimwengu utuibie uwepo wake na kutuacha kama yatima; haya yalitokea kwa faida na manufaa yetu! Haki inafunua kuwa Mungu aliukombo utambulisho wa kweli wa mwanadamu, na kufanikiwa kurejesha hali ya kuwa bila hatia. Mfano na sura ya Mungu kwa mara nyingine tena ilifunuliwa katika mwili wa mwanadamu. Mwili wa mtu na nafsi sasa ni makao matakatifu ya Mungu. Chembe ya ngano haikubaki peke yake, ilianguka katika nchi na kufa, na kufufuka katika mavuno ya makundi ya watu ambao maisha yao na miili yao, vinazidisha uwepo na kusudi la Mungu ulimwenguni. Kufanyika mwili hakukuishia kwa Yesu tu; Neno lile ambalo ni Mungu, sasa limezidishwa ndani yetu! Tumekuwa katika utimilifu wa uzima ndani yake. Yoh. 1:14,16; Kol. 2:9,10. "Kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu." 1Yoh. 4:17. "Lililo kweli ndani yake, ni kweli ndani yetu pia" 1Yoh. 2:8. Ndiyo sababu haki ipatikanayo kwa imani yanena hivi, "Usiseme moyoni mwako, Ni nani atakayepanda kwenda mbinguni? Yaani ni kumsihi Mungu amrudishe Kristo duniani; au ni nani atakayeshuka kwenda kuzimuni, yaani ni kumleta Kristo juu kutoka kwa wafu. Lakini yanenaje? Haki ambayo ni matokeo ya imani inasema, Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako na katika moyo wako." Haki inafunua na inaelewa kuwa sisi tumefufuliwa pamoja naye katika ulimwengu wa roho! Sisi ni uwepo wake hapa duniani! Umbali kati yetu ulifutwa! Neno lake haliko karibu mbinguni au mamlaka makubwa kule kuliko lile lililo katika vinywa vyetu na mioyo yetu katika sayari ya dunia hii! Rum. 10:2-8.

Jambo la tatu ambalo Roho Mtakatifu anashauri ulimwengu kwa ajili ya hukumu; "Kwa sababu mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa!" Yesu alipoangikwa msalabani, mwili wa kibinadamu ulitundikwa pale kama hati ya mashitaka. Hivyo hitaji la sheria lilitimizwa. Vyanzo vyote vya mashitaka vilishughulikiwa katika kifo chake. Injili inatangaza kwamba mshitaki wa wanadamu alivuliwa kwa silaha zake. Neno la Kigriki ni, *satanos*, maana yake mshitaki. Silaha yake ilikuwa ni hatia ya mwanadamu. Kol. 2:14,15. Ndipo imekuwa dhahiri kwamba kuendelea kumwona mwanadamu kuwa najisi, na mwenye dhambi asiyekombolewa, ni kuudharau msalaba, na kuendelea kumpa nguvu adui ambaye tayari alikwisha kushindwa.

"Nasi na tujue, naam, tukaendeleo kumjua Bwana; sawasawa na kujumlishwa kwa mwanadamu katika kifo na kufufuka kwake." Hos. 4:6; 6:2,3.

#### KIPINDI KIPYA?

Ukweli kama ulivyo katika Kristo, haujawahi kamwe kutishiwa na uongo wa kipimo chochote. Ef. 4:20,21.; 2Kor. 13:4,8. Uliandaliwa kuijua kweli. Kweli yenyewe haiwezi kukuweka huru, bali, "MTAIFAHAMU kweli, na hiyo kweli itawaweka huru!" Roho wa Mungu ni Roho wa kweli, naye hushuhudia ndani yetu pamoja na roho zetu kwamba sisi ti wana wa Mungu. Analia pamoja nasi Abba, yaani Baba! "Nasi twajua

kwamba Mwana wa Mungu amekwisha kuja, naye ametupa akili kwamba tumjue yeye aliye wa kweli, NASI TUMO NDANI YAKE yeye aliye wa kweli!" 1Yoh. 5:20. Haya siyo mafundisho mageni, bali ni Neno la Mungu lililokuwako tangu mwanzo. Hata hivyo ni amri mpya, katika hiyo sasa tunajua kwamba lililo kweli ndani yake, vile vile ni kweli ndani yetu. 1Yoh. 2:7,8.

Kipindi kipya ni chapa ya filofia ambayo mara nyingi wakristo wanaiunganisha na chochote kionekano kuwa ni kigeni kwa mafundisho ya desturi yanayokubaliana na hukumu, na hali ya dhambi ya mwanadamu! Wakristo wengi husema amina hakika kwamba mwanadamu ni mfidadi na mwenye dhambi, lakini wameichukia Habari Njema yenye matokeo ya kujumlishwa kwa mwanadamu katika Kristo. Wanajitahidi kuamini kitu ambacho bado hawawezi kukiona! Mwanadamu bado anaangalia dhambi na magonjwa, kwa hiyo, tunathubutuje kumtangazia kuwa hana hatia na ameponywa? Inakuwa kama yaliyotokea kwa mwanadamu katika Adamu yanabeba uzito mkubwa zaidi, mamlaka na msukumo juu ya mtu, kuliko yaliyotokea kwetu katika Kristo! Rum. 5:14-21. Wanakubali kuwa mwivi huja tu kuiba, kuu na kuharibu, lakini wanashindwa kusoma au kuamini kuwa sehemu ya pili ya msitari huo katika Yohana 10:10, ndio hasa maana ya Agano jipya lote! Unasema, BALI mimi nimekuja ili MWE na uzima, kasha mwe nao tele! Habari Njema ni tangazo linalokubalika sana kuhusu mwanadamu, ambalo linaweza kutangazwa daima.

Kipindi kipya na U-buddha ni filofia inayokubalika sana, bali wanashindwa kuona na kuelewa maana ya Yesu. Yesu sio mmoja wa wana filofia mwingine; Yeye ni Mungu Muumbaji katika mwili dhaifu au kiini macho! Yeye ni Neno la milele aliyefanyika mwili. Amemfanya Mungu asiyeonekana aonekane! Pia ni chapa yetu ya mpango wake wa asili, Mungu aliposema, "Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu!" Yeye ndiye peke anayestahili kuwakilisha Uungu na ubinadamu katika nafsi moja! Kol. 2:9,10. Kifo, kuzikwa na ufufuo wa Yesu, na kujumlishwa kwa mtu ndani yake, hakufundishwi katika katika mafundisho ya Kipindi Kipya. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba hata mahali ambapo kumbukumbu za kihistoria za kifo na ufufuo wa Yesu zinafundishwa katika mzunguko wa desturi za kikristo, hazina nguvu sawasawa na Filofia yoyote ya Mashariki; mpaka ufunuo wa kuunganishwa kwa mwanadamu katika Kristo kumeonekana na kutangazwa. Imani na ukombozi wa kweli unakuja tu kwa njia ya ufunuo wa Kristo! Rum. 10:17; 1Kor. 2:6-8.

Lile Neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako. Neno ni kiongozi wa maisha yako. Kweli haipimwi kwa kuwapo au kukosekana kwa hisia, wala kweli haipingwi kwa upinzani au nia ya umbali. Mungu hawi karibu wakati fulani, na wakati mwingine kuwa mbali; hawezi kuwa Imanueli kwa siku maalumu, na siku nyingine hapana. Yeye ni Imanueli wa milele! Mungu yuko pamoja nasi, na kwa ajili yetu, na ndani yetu! Ndani yake tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Hupumui tu kwa wakati, au wakati unapoelewa kufanya hivyo! Unapumua wakati wote, hata unapokuwa usingizini. "Kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote, naye hayuko mbali na kila mmoja wetu." Mdo 17:24-28.

Sasa, "Ili kwamba ushirika wa imani yako ufanye kazi yake, katika ujuzi wa kila kitu chema kilicho kwetu katika Kristo." Filem. 6. Mtazamo huu peke yake ndio ushirika wa kweli! Tuna usalama hapo; mbali na masengenyo au sifa mbaya. Tunaweza sisi wenyewe kwa furaha kufikiri na kunena mawazo yake yanayotuhusu sisi pekee!

© Copyright 2010 — Francois du Toit. The detailed copyright notice can be viewed here:

[http://www.mirrorword.net/Resources\\_Teachings/Your\\_Right\\_to\\_Copy](http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Your_Right_to_Copy)

(You may freely copy, but not sell, make any changes or claim/imply ownership of any portion or the whole of the text)

Note, all material on the mirrorword.net site is FREE of charge:

1. Read how the Mirror revelation – knowing Jesus as in a mirror - is totally transforming people and nations:

[http://www.mirrorword.net/About\\_Us/Testimonies](http://www.mirrorword.net/About_Us/Testimonies)

2. The MirrorWord bible translation (a definite MUST HAVE) – the best grace-based translation of the bible from the original languages!

[http://www.mirrorword.net/Resources\\_Teachings/MirrorWordBible](http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/MirrorWordBible)

(Knowing Jesus as in a mirror and the significance of the cross is the key to understanding the bible)

3. Subscribe yourself or others (they can unsubscribe) for a short & powerful daily revelation sent to your email address:

[http://www.mirrorword.net/Daily\\_Thoughts](http://www.mirrorword.net/Daily_Thoughts)

4. Audio and video teachings of wordschools and selected teachings:

[http://www.mirrorword.net/Resources\\_Teachings/Audio](http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Audio)

[http://www.mirrorword.net/Resources\\_Teachings/Video](http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Video)

5. Various books and shorter teachings to download and read:

[http://www.mirrorword.net/Resources\\_Teachings/Books\\_Magazines](http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Books_Magazines)

[http://www.mirrorword.net/Resources\\_Teachings/Articles](http://www.mirrorword.net/Resources_Teachings/Articles)

6. Study material for groups/individuals and books and a lot more:

[www.scribepublishing.co.za](http://www.scribepublishing.co.za)

7. The material is being translated in many other languages (you're welcome to help!)

[http://www.mirrorword.net/1Other\\_Languages](http://www.mirrorword.net/1Other_Languages)

8. Join the rich and wonderful grace discussions online:

[www.facebook.com/mirror.reflection.net](http://www.facebook.com/mirror.reflection.net)

[www.facebook.com/francois.toit](http://www.facebook.com/francois.toit)

9. Join the online school of grace – amazing place where people's lives are being transformed in a friendly environment:

[www.schoolofgrace.net](http://www.schoolofgrace.net) (or email [andre.rabe@gmail.com](mailto:andre.rabe@gmail.com)).

10. Check out the following addresses for more of the Mirror revelation:

[www.scribepublishing.co.za](http://www.scribepublishing.co.za)

[www.hearhim.net](http://www.hearhim.net)

More links: [http://www.mirrorword.net/About\\_Us/Links](http://www.mirrorword.net/About_Us/Links)

11. How you can get involved with biblestudy groups etc.:

[http://www.mirrorword.net/Get\\_Involved](http://www.mirrorword.net/Get_Involved)

Enjoy - you were made for it!

12. If you desire to make donations towards the ministry to help others hear the good news... We are a registered Non-profit organisation:  
[http://www.mirrorword.net/Get\\_Involved](http://www.mirrorword.net/Get_Involved)